

SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI UUZWAJI WA NYUMBA ZA LEVOLOSI, ARUSHA

Kwa mara nyingine tena Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) leo (Jumapili, 9, Septemba, 2012) limezindua rasmi mauzo ya nyumba katika mradi wake mpya wa Levولي، jijini Arusha. Ujenzi wa mradi huo ulianza rasmi mwezi Januari mwaka huu (2012) na unatarajiwa kukamilika rasmi Januari 2013.

Mradi huu upo eneo la Levولي kweye barabara ya kuelekea Ngarenaro na Nairobi karibu kabisa na Chuo cha Ufundı cha Arusha (Arusha Technical College) na zitakuwa sehemu moja na nyumba za Shirika la Nyumba za Levولي. Mradi huu uko sehemu unazo huduma zote muhimu za kijamii jijini Arusha zikiwamo za kiafya, shule, maduka, na masoko.

Pia Mradi huu unatarajiwa kuboresha maisha ya wanunuzi wa nyumba hizi kwani upo karibu kabisa na katikati ya jiji, nyumba zipo ndani ya uzio kwa ajili ya usalama wao na kuna maegesho ya magari ya kutosha.

Mradi una nyumba 100 tu zinazouzwa, kila nyumba ina vyumba viwili vya kulala, kimoja kati ya hivyo ni cha kulala kinachojitegemea. Kila nyumba ina ukubwa wa mita za mraba 60 (sq.m), sebule iliyoungana na eneo la kula chakula, choo cha umma, jiko kubwa la kisasa na eneo la kufulia na kuanikia nguo. Sifa za ziada za mradi huu ni kuwa na eneo la watoto kuchezza, eneo maalum la kukusanya taka, maegesho ya magari ya ziada.

Kila nyumba itauzwa kwa bei ya **Sh TZS 82,108,882.21 Bila VAT.**

Tunawahamasisha na kuwakaribisha watanzania wote walio nchini na wasio wafanye mawasiliano na makao makuu ya shirika, ofisi zetu za mikoa, au kupitia barua pepe na kukamilisha taratibu mapema kwa ajili ya kuweza kuingia kwenye mchakato ulio wazi wa manunuzi.

Uzinduzi wa mauzo ya nyumba za mradi huu ni mfululizo wa uzinduzi wa miradi ya NHC unaolenga kutimiza malengo ya mkakati wa Shirika wa miaka mitano ya kujenga nyumba 15,000 ambazo kati ya hizo, nyumba 10,000 ni za wananchi wa kipato cha kati na cha juu na 5,000 kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini.

Ukiwa mdau na mnunuzi mtarajiwa, ama una ndugu/rafiki anayetamani kununua nyumba katika mradi huu, tafadhalii waweza tumia akaunti nambari : **011103002716-NATIONAL HOUSING CORPORATION. Bank : NBC. Branch : CORPORATE BRANCH** au wasiliana na kitengo cha mauzo **simu namba 0754 444 333;** **barua pepe:** **sales@nhctz.com** na pia tembelea tovuti ya shirika **www.nhctz.com** kwa maelezo zaidi.

IMETOLEWA NA:

KITENGO CHA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA JAMII

SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA